



P.O. Box 21522, Dar-es-Salaam, Tanzania Tele/Fax: +255 (0) 22 2669007 Email: info@mjumita.or.tz

TANGAZO LA ZABUNI

Zabuni Na: 01/MJUMITA/2024

Tarehe ya kutolewa: 10/10/2024

Mwisho wa kutuma maombi: 24/10/2024

I. Utangulizi

Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) ni shirika lililokuwa la kiserikali lililoanzishwa mwaka 2007 na lenye Namba ya usajili 00NGO/R1/00902. MJUMITA imeundwa na mitandao (Vikundi vinavyojihusisha na usimamizi wa misitu) takribani 132 kutoka vijiji 453, wilaya 36 na mkoa 16 ya Tanzania bara. Mitandao ya MJUMITA inajihusisha na usimamizi wa misitu, ufugaji nyuki, utengenezaji wa mkaa endelevu pamoja na vikundi vya kuweka na kukopa ambao wanasimamia misitu takribani hekari milioni 1.8. Kupitia mradi wa kuimarisha vikundi vya uzalishaji wa mazao ya misitu na kilimo, MJUMITA inatangaza zabuni kutoka mafundi wenye sifa kwa ajili ujenzi wa kituo kidogo cha kuchakata asali katika kijiji cha Maguha kilichopo Wilaya ya Kilosa, Mkoa wa Morogoro.

2. Mchanganuo wa jengo

Kituo kidogo cha kuchakata asali kitakuwa na vyumba vye vipimo vifuatavyo:

Na	Chumba	Ukubwa
1	Chumba kimoja cha kuchakata asali	(6x8)m
2	Stoo ya kuhifadhi asali ghafi	(6x3)m
3	Chumba cha duka la asali	(3x3)m
4	Ofisi	(4x4)m
5	Ukumbi wa mikutano	(4x6)m

3. Eneo la kazi

Ujenzi utafanyika katika kijiji cha Maguha wilaya ya Kilosa ambapo mzabuni atayekidhi vigezo atafanya shughuli za ujenzi na kukabidhi kituo kilichokamilika kwa shirika la MJUMITA.

4. Vigezo vinavyohitajika

Wazabuni wote lazima wawe na vigezo vifuatavyo:

- Cheti halali cha usajili wa biashara
- Awe amesajiliwa kwenye mfumo wa kulipa kodi (EFD receipt registered)
- Uzoefu wa kufanya kazi kama hizi kwa miaka isiyopungua 10

d) Uwezo wa kifedha wa kushughulikia mradi

5. Mahitaji muhimu ya kuwasilisha

Wazabuni wataambanisha nyaraka zifuatazo kwa MJUMITA:

a) Andiko la kiufundi la mradi ya ujenzi wa kituo kidogo cha kuchakata asali

b) Nakala ya leseni ya biashara

c) Mchanganuo wa gharama za utekelezaji wa mradi

6. Jinsi ya kutuma maombi

Wazabuni wanatakiwa kutuma maombi yao (Mapendekezo/andiko la mradi na mchanganuo wa gharama kwa ofisi ya manunuzi ya MJUMITA) kupitia barua pepe info@mjumita.or.tz na nakala dlukas@mjumita.or.tz yenye maandishi yafuatayo "Zabuni ya ujenzi wa kituo cha kuchakata asali" ifikapo tarehe 24/10/2024 saa 23:59 usiku.

7. Kufungua zabuni

Zabuni zitafunguliwa mbele ya wawakilishi wa wazabuni watakaoweza kuhudhuria siku ya tarehe 25 Oktoba, 2024, saa 03:00 katika ofisi za MJUMITA, Dar es Salaam.

8. Mawasiliano

Kwa taarifa zaidi, wasaliana na MJUMITA kupitia anuani ifuatayo
MJUMITA,
S.L.P 21522,
Dar es Salaam.
0768636735

MJUMITA haki ya kukubali au kukataa zabuni yoyote bila kutoa sababu kwa mzabuni husika.

Imeandaliwa na:

Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misititu Tanzania (MJUMITA)

10/10/2024